# UTUREHEMU EE BWANA


Na: B.P. MWANDU
NYEGEZI-MWANZA
22/01/2018

Lento

*Zab. 51:1-4,10-12, 15 (K) 1*




Maimbilizi



1.Ee Mungu unirehemu sawasawa na fadhili zako/ kiasi cha wingi wa rehema zako,
uyafute makosa yangu// Unioshe kabisa na uovu wangu,unitakase dhambi zangu.

2.Maana nimejua mimi makosa yangu, na dhambi yangu i mbele yangu daima/
Nimekutenda dhambi wewe peke yako// na kufanya maovu mbele ya macho yako.

3.Ee Mungu uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu/
Usinitenge na uso wako// wala roho yako mtakatifu usiniondolee.

4.Unirudishie furaha ya wokovu wako, unitegemeze kwa roho ya wepesi/
Ee Bwana uifumbue midomo yangu// na kinywa changu kitazinena sifa zako.

Printed by BoltPDF (c) NCH Software. Free for non-commercial use only.